



Bunty na Bubbly

Bunty anapenda kucheza na vipepeo...




... na ndege.



Anapenda kucheza na mashua iliyotengenezwa kutoka kwa makaratasi.



Anapendelea pia kutengeneza mangome kutumia changarawe.



Bunty anaporudi nyumbani, mamake humuuliza ajisafishe.
Lakini hukataa.



“Nachukia sabuni!” yeye hulia.



Usiku mmoja, alikuwa na ndoto.

Aliota kuwa vijidudu vinavyosababisha magonjwa vilikuwa vimeizunguka ngome yake na vilikuwa vinamvamia.




Bunty anafukuzwa na vijidudu.

Anakimbia kuokoa uhai wake huku akipiga mayowe, "Nisaidie...Nisaidie!"



Ghafla, Mfalme Sabuni kwa jina Bubbly anatokezea. “Bunty, usiogope,” anasema. “Nenda mkavamie vijidudu!” Mfalme Sabuni anaamrisha jeshi lake la povu.



Jeshi la povu linafukuzia mbali vijidudu.



Siku hizi, Bunty hupendelea kutumia sabuni, na hujipangusa na kujisugua hadi anakuwa msafi.

